



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

JIMBO LA TABORA MJINI

HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA



Kumb. Na. TMC/U/19/82

Tarehe 04.03.2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Tabora Mjini kwa kuzingatia kanuni ya 12 na 13 za Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za watendaji wa vituo vya kupigia kura kwa ajili ya uchaguzi mdogo utakaofanyika tarehe 20 Machi, 2024 katika Kata ya Ndevelwa kama ifuatavyo: -

1. **Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura Nafasi 16**
 2. **Msimamizi Msaidizi wa Kituo cha Kupigia Kura Nafasi 32**
 3. **Karani Mwongozaji Wapiga Kura Nafasi 16**
- A. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA**
- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
 - (b) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;
 - (c) awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
 - (d) Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kusoma na kuelewa kitabu cha Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na
 - (e) Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo anaomba kufanya kazi.
- B. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA KARANI MWONGOZAJI WA WAPIGA KURA**
- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
 - (b) Awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kuongoza wapiga kura;
 - (c) Ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo atakachofanyia kazi;
 - (d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;

- (e) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuelewa kitabu cha Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na
- (f) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo: -

- i. Siku ya Uchaguzi Msimamizi wa Kituo atalipwa posho ya Shilingi **60,000** kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Shilingi **10,000** kwa siku moja na nauli Shilingi **20,000**.
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Shilingi **50,000** kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Shilingi **10,000** kwa siku moja na nauli Shilingi **20,000**;
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Shilingi **50,000** kwa siku moja na posho ya chakula Shilingi **10,000**.
- iv. Wakati wa mafunzo watendaji wote watalipwa posho ya Shilingi **50,000** na nauli Shilingi **20,000** kwa kila siku ya mafunzo. Mafunzo kwa wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa vituo yatafanyika kwa muda wa siku mbili, na mafunzo kwa makarani waongozaji wapiga kura yatafanyika kwa muda wa siku moja.

D. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE

- i. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
- ii. Maombi yote yaambatishwe na vyeti vya taaluma, nakala ya vyeti vya kidato cha nne, kidato cha sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa alizonazo kwa mujibu wa Tangazo hili.
- iii. Waombaji waambatishe picha mbili zenye ukubwa sawa na picha iliyopo kwenye pasi ya kusafiria (Passport size) za hivi karibuni.
- iv. Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma wapitishwe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
- v. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria endapo watabainika.

Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ya kazi ni tarehe 10 Machi, 2024.

Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni: -

Msimamizi wa Uchaguzi,
Jimbo la Tabora Mjini,
S. L. P 174

TABORA

Limetolewa na:-



Elias M. Kayandabila
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA TABORA MJINI